Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Majivuno na Kiburi.

949. **Al Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s.** amesema**,** *Tasnif-i-Ghurar-ul-Hikam,Uk. 443:*

"Msiwe wakaidi (na msing'ang'anie kufuata vile mfikiriavyo nyie wenyewe), kwa sababu watu kama hawa hukumbana na maangamizo."

950. **Al Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s.,** amesema *Tasnif-i-Ghurar-ul-Hikam,Uk. 308 na Bihar al-Anwaar, J. 6, Uk. 91:*

"Yeyote yule ajionaye kuwa yeye ndiye mkubwa kabisa (hana mfano mwingine) basi si kitu chochote kile mbele ya Allah swt."

951. **Al Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s.** amesema**,** *Bihar al-Anwaar, J. 72, Uk. 39:*

"Mambo mawili yanasababisha watu kuangamia (na kutumbukizwa katika Jahannam):
- *Kuogopa umaskini, na*
- *Kutaka ukubwa kwa kupitia majivuno."*

952. **Al Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s.** amesema**,** *Ghurar-ul-Hikam, Uk. 298:*

"Mjiepushe na kujifakharisha wenyewe, kwa kutegemea yale muyaonayo mazuri ndani mwenu na kwa kupenda kuzidishiwa sifa kwa sababu hayo ndiyo majukumu makubwa yakutegemewa na Shaytani."

953. **Al Imam Ja'afer as-Sadiq a.s.,** amesema *Al-Kafi, J. 2, Uk. 310:*

"Yeyote yule aliye na kiburi hata kidogo moyoni mwake basi hataruhusiwa kuingia Jannah."

Source URL:
https://www.al-islam.org/sw/hadith-za-mtume-s-na-ma-imamu-700-1710-amiraly-m-h-datoo/majivuno-na-kiburi#comment-0